BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

FEBRUARI, 2024

MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA

OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
KWA MWAKA WA FEDHA 2023 – 2024

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote napenda kutumia fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mjuzi wa yote, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vilivyomo, kwa kutujaalia afya njema iliyotuwezesha kukutana tena siku ya leo katika Baraza hili Tukufu kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu kwa mustakabali ulio bora. Aidha, namuomba Mwenyezi Mungu azidi kutuongoza ili tuweze kujadili mambo muhimu ya maendeleo ya Taifa letu na kutekeleza majukumu ya kazi za kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** ninamshukuru tena Mwenyezi Mungu (SW) kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano, hali ambayo imeendelea kuipa nafasi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wananchi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Napenda kuwasisitiza viongozi pamoja na wananchi kwa ujumla kuendelea kudumisha kikamilifu amani na utulivu tulionao kwani bila ya amani na utulivu hakuna maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa dhati kabisa napenda kumpongeza na kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake, pia kujali kwake Utawala wa Sheria na Utawala Bora katika kipindi chote tokea ashike wadhifa wa kuiongoza nchi yetu. Aidha, Kamati inampongeza Mhe. Rais kwa kufanikisha vyema Maadhimisho ya Sherehe za kutimiza miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, zilizotanguliwa na ufunguzi wa miradi mingi sana na mikubwa ya maendeleo pamoja na kuweka mawe ya msingi kwa baadhi ya miradi inayoendelea kujengwa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu na afya ya kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha muhtasari wa Ripoti ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ripoti ambayo inaonesha shughuli zote ambazo tumezitekeleza katika kipindi hiki.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima, kupitia Ofisi zinazosimamiwa na Kamati yetu napenda kuelekeza salamu zangu za pongezi kwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdalla, kwa juhudi na maarifa yao ya kumshauri ipasavyo Mheshimiwa Rais wetu mpendwa hadi tukaweza kufikia hatua kubwa ya mafanikio. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo huo na awajaalie maisha marefu yenye kheri na baraka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inaungana na familia, ndugu, jamaa na watanzania wote kwa ujumla kufuatia msiba wa Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kilichotokea katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete Dar es Salaam siku ya Jumamosi, tarehe 10 Februari 2024, tunamuomba Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema anapostahiki, Amin.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambayo imeundwa na kupewa majukumu kwa mujibu wa kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Kanuni ya 107 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka 2020 maelezo zaidi kuhusu majukumu ya Kamati hii, yameelezwa katika jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la Mwaka 2020. Kadhalika kwa mujibu wa kifungu cha 109 (15) cha kanuni hiyo inazitaka Kamati za Kudumu kuwasilisha Ripoti ya Shughuli zake ndani ya Baraza katika Mkutano wa Mwezi wa Febuari.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti hii inaakisi kazi za Kamati ambazo zimefanywa

kuhusiana na utekelezaji wa Taasisi zilizo chini yake kwa kipindi cha mwaka wa fedha, 2023/2024 na kwa kuzingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ambayo inajumuisha Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 – 2025.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufuatilia utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2023/2024. Kamati imepewa jukumunla kusimamia wizara tano ambazo ni Ofisi ya Rais – Ikulu; Ofisi ya Makamu wa wanza wa Rais; Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika,** Shukurani za pekee ziwaendee Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano makubwa ambayo yameiwezesha kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi na uzoefu mkubwa na hatimae kukamilika kwa ripoti hii. Napenda sasa kuwatambua kwa majina Wajumbe wanaounda kamati hii kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Maryam Thani Juma | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Panya Ali Abdalla | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii inafanyakazi chini ya uratibu wa Makatibu watatu na

Mkalimani wa lugha za alama mmoja ambao kwa pamoja wamekuwa msaada mkubwa katika kufanikiza majukumu ya kamati hii, kwa kutumia maarifa na weledi wa hali ya juu katika shughuli za kamati. Makatibu hawa ni:

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg. Ali alawy Ali | - | Katibu |
| 2. Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | - | Katibu |
| 3. Ndg. Shawana Mohammed Haji | - | Katibu |
| 4. Ndg. Amina Abeid Hemed | - | Mkalimani wa lugha za alama |

**Mheshimiwa Spika**, naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kufahamu kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa jumla kwa kila Wizara. Hivyo, maelezo zaidi na kwa ukamilifu yanapatikana katika ripoti ambayo tayari inaonekana katika vishkwambi vya Waheshimiwa Wajumbe. Vile vile, katika kipindi hiki kamati ilifanya kazi zake katika mizunguko mitatu (3) kwa muda wa wiki Tisa (09) katika utaratibu uliojipangia kwa Unguja, Pemba na Tanzania Bara.

## 2. MAUDHUI YA KAZI ZA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeeleza kwa kina utekelezaji wa shughuli zilizofanywa na wizara ambazo zinasimamiwa na kamati kama nilivyozitaja hapo juu kwa kupokea taarifa tofauti za kila robo ya mwaka (quarterly reports) katika utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya taasisi husika, kupokea taarifa za utekelezaji wa maagizo ya kamati katika mwaka uliopita, kukutana na wadau mbali mbali wa sekta za umma, pamoja na kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo ili kuona hatua na mafanikio ya utekelezaji wa sekta hizo zimefikiwa. Sambamba na hayo, kamati ilifanya kazi ya kupitia miswada na taarifa mbali mbali za Serikali kwa kila Mkutano wa Baraza ulipofanyika. Maelezo zaidi ya miswada na taarifa za Serikali yanapatika Ukurasa wa 7.

**MheshimiwaSpika,** kiujumla, kamati imeridhishwa na kasi ya maendeleo ya Serikali ya Awamu ya Nane pamoja na utekelezaji bora wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa Taasisi zote ambazo zinasimamiwa na kamati hii kutokana na kukamilika kwa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inatekelezwa na Serikali.

## 2.1 OFISI YA RAIS – IKULU

**MheshimiwaSpika,** utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais Ikulu yameleezwa vyema kupitia Ukurasa wa 10 hadi 13 katika kitabu cha Ripoti. Aidha, kamati inatoa pongezi za dhati kwa Ofisi ya Rais Ikulu kutokana na mafanikio mbali mbali yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2023/2024. Kwa fursa hii, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri katika Ofisi hii Mhe. Ali Suleiman Ameir kwa uteuzi wa nafasi yake mpya na kwa mashirikiano ambayo ameyatoa kwa kamati muda mfupi baada ya uteuzi wake. Kwa kufupisha maneno tunasema kamati imeridhika na namna Ofisi inavyotekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024 kamati imefanya ziara kwa viongozi wastaafu mbali mbali wa nchi akiwemo Mheshimiwa Dkt. Amani Abeid Karume, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, kwa lengo la kufahamu changamoto na kuishauri Serikali kutafuta namna bora ya kuzipatia suluhisho. Aidha, Kamati imepata kujifunza masuala ya ukuzaji diplomasia ya nchi pamoja na kupata uzoefu wao kwenye masuala ya uongozi na kuendelea kuwaenzi viongozi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imejiwekea utaratibu wa kuwatembelea wastaafu hao mara kwa mara kwa kuwa inatambua michango yao mikubwa katika kuitumikia nchi kwa vipindi vyote vya utumishi wao wa umma. Kwa mantiki hiyo, kamati inaishauri Serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Maslahi ya Viongozi Wakuu wa kitaifa ili kuendelea kuyatetea, kuyasimamia na kuyalinda maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaipongeza Serikali kwa kujali na kuboresha maslahi ya wafanyakazi kupitia taasisi mbali mbali za umma kwa lengo la kuwapunguzia ukali wa maisha. Hata hivyo, tunaishauri Serikali kuangalia zaidi maslahi ya watendaji wa Ikulu pamoja na Baraza la Mapinduzi kutokana na unyeti wa kazi wanazozitekeleza

kwani kwa muda mrefu maslahi yao hayajafanyiwa mapitio.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaishauri Serikali kupitia Taasisi ya Nyaraka na Kumbumbu za Taifa kuongeza mashirikiano baina ya Taasisi za Umma na binafsi kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu na kutunza historia ya Zanzibar. Maelezo zaidi kuhusu Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa yanapatikana Ukurasa wa 12 hadi 16. Aidha, kamati inashauri wakuu wa taasisi kutilia uzito suala la uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu kwa ajili ya matumizi ya baadae.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaipongeza Taasisi ya Nyaraka kwa kufanikiwa kununua nyumba za karibu na ofisi za Nyaraka Kilimani na hivyo kuweza kutanua eneo la kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi mpya. Aidha, kamati inaishauri Serikali kuharakisha taratibu za ujenzi wa ofisi hii kutokana na kuwepo kwa changamoto mbali mbali katika jengo linalotumika kwa sasa, ikiwa ni pamoja na kutafuta eneo jengine kwa ajili ya ujenzi wa ofisi mpya ya Nyaraka kisiwani Pemba.

## 2.2 OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

**MheshimiwaSpika,** maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2023/2024 yanapatikana kuanzia Ukurasa wa 21 hadi 35 hii pamoja na kusimamia idara mbali mbali, pia inajukumu la kusimamia na kuratibu Ofisi ya Faragha ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na masuala ya Sera, Mipango na Tafiti za Ofisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, kamati imeridhika na utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais kwa kutekeleza vyema Mipango, Sera na Miongozo ya Serikali kwa lengo la kutimiza wajibu wake. Kamati inampongeza kwa dhati kabisa Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Massoud Othman kwa namna anavyotekeleza majukumu yake na kuhakikisha Zanzibar inapiga hatua ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaipongeza Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa kufanikiwa kutekeleza vyema majukumu ya kusimamia na kutunza mazingira. Aidha, kamati inashauri ZEMA kuendelea kutoa elimu juu ya namna bora ya matumizi endelevu ya rasilimali zisizorejesheka kwa kuishauri Serikali kufikiria njia mbadala ya kufanya kwa wakaazi wa maeneo ya Micheweni ambao wamejikita katika shughuli za ukataji wa matofali na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Katika hali hiyo, kamati inatoa wito kwa jamii kuyalinda mazingira yetu kwa kuepuka kufanya kazi ambazo zinaweza kusababisha majanga makubwa katika nchi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inashauri Mamlaka ya ZEMA kushirikiana na Idara ya Mazingira kuzidisha kasi ya mradi wa ujenzi wa tuta la kuzuia maji chumvi eneo la Sipwese katika Wilaya ya Mkoani na kuwashauri wahisani wa mradi huu kuongeza kasi ya mradi kabla ya kipindi cha mvua kubwa za masika.

**Mheshimwia Spika,** kwa upande mwengine, kamati imebaini uwepo wa muhali kwa wananchi katika kushirikiana na Mamlaka kutoa taarifa na ushahidi dhidi ya vitendo vya dawa za kulevya katika jamii kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Zanzibar ya Mwaka 2022 na 2023. Aidha, kamati inashauri Serikali kuielimisha jamii umuhimu wa kutoa mashirikiano na taasisi husika kwa lengo la kufichua na kutoa taarifa za wahalifu wa dawa za kulevya kwa maslahi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, kamati inasikitishwa kuona taasisi za haki jinai zenye wajibu wa kusimamia kesi za dawa za kulevya zinawaachia na kutowachukulia hatua stahiki wahalifu kwa kisingizio cha kukosekana ushahidi huru, jambo ambalo linaifanya jamii kuiona Serikali inatoa fursa kwa wahalifu kuzidisha kasi ya uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya na hivyo jamii kuathirika zaidi kwa kuwapoteza vijana wa rika tofauti.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaishauri Mamlaka ya Dawa za Kulevya kuimarisha

programu za kutoa elimu kwa jamii juu ya kujitambua na kutoa mafunzo kwa watoto wa Skuli za Msingi na Sekondari. Juhudi hizi ziende pamoja na ushirikiano baina yao na wazazi ili kuendelea kuwapa taaluma ya malezi bora watoto na kuwafahamisha juu ya athari za dawa za kulevya katika maisha.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaishauri Serikali kutumia nguvu kubwa ya kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuwatunza na kuwalinda waathirika wa dawa za kulevya wakati wanapoacha kutumia dawa na kuwa wananchi wema katika jamii. Pamoja na hilo, kamati inaitaka Serikali kutafuta uwezekano wa kujenga nyumba za waraibu wa dawa za kulevya iliyo salama na kuachana na nyumba za kukodi ambazo zipo katikati ya makaazi ya watu kisiwani Pemba. Sambamba na kuongeza kasi ya uratibu wa ujenzi wa nyumba ya uraibu kwa upande wa wanawake katika eneo la Kangagani Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imebaini kuwepo kwa uhaba na ufinyu wa ofisi kwa Idara ya Watu wenye Ulemavu Pemba jambo ambalo linakwaza shughuli zao. Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kuwawezesha kwa misaada taasisi hii pamoja na kuwaandalia mazingira wezeshi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao kwa urahisi na kupata maslahi yatakayosaidia kujenga maisha yao. Maelezo zaidi kuhusu Idara ya watu wenye ulemavu yanapatikana Ukurasa wa 34 na 35.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Tume ya Ukimwi Zanzibar, Kamati imebaini ofisi kukabiliwa na uhaba wa fedha ambazo hupelekea kushindwa kutekeleza shughuli ilizopanga. Hata hivyo, shughuli nyingi zilizotekelezwa ni zile zinazogharamiwa na Washirika wa Maendeleo ambazo hazitoi nafasi ya kutekeleza programu zinazolenga jamii moja kwa moja na kuathiri upatikanaji wa huduma mbali mbali za UKIMWI. Sambamba na hilo, Kamati imebaini kuongezeka kwa tabia hatarishi zinazoweza kuchochea maambukizo ya VVU hasa kwa jamii ambazo zinahitaji muitiko wa kijamii na kisera katika kupambana nazo.

**Mheshimiwa spika**, kwa mnasaba huo, Kamati inaishauri Serikali ioneshe wajibu wake kupitia mapambano dhidi ya UKIMWI badala ya kusubiri wafadhili wa mashirika. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya Sera na Sheria ya

Ukimwi ili kuweka taraatibu za kisheria za kuwepo kwa mfuko maalumu wa UKIMWI Zanzibar.

## 2.3 OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

**Mheshimiwa Spika,** maelezo kuhusu mafanikio, changamoto, maoni, mapendekezo na ushauri kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yanapatikana kuanzia Ukurasa wa 36 hadi 46 Kwa kuwa jukumu la msingi la Ofisi hii ni kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na masuala ya Muungano kwa upande wa Zanzibar. Ofisi hii pia, inasimamia Taasisi mbili zinazojitegemea ambazo ni Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (BLW) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC). Kwa ufupi kamati imeridhika na utendaji wa Ofisi kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao na kuimarisha hali ya nchi yetu.

**MheshimiwaSpika,** kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kufuatilia na kusimamia taasisi za umma katika kutoa huduma bora na kuhakikisha kuwa miongozo na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara ya kamati Dodoma, tulibaini kuwepo kwa changamoto mbali mbali katika ofisi ya Uratibu wa SMZ jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi za kila siku. Kamati inaishauri Serikali kuiboresha ofisi ya Dodoma na ofisi ndogo ya Dar es Salaam kwa kupatiwa nyenzo muhimu za utendaji pamoja na kuangaliwa suala la kuongezewa watendaji wenye uwezo wa kufanya kazi kwa uzalendo na kujitolea. Sambamba na hilo, kamati inaomba Serikali kutatua changamoto ya usafiri kwa ofisi ya Dodoma kutokana na uhaba na uchakavu wa gari wanazotumia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Kamisheni ya Maafa Zanzibar, kamati inaishauri Serikali kuanzisha mfuko wa maafa ambao utaiwezesha Kamisheni kutekeleza shughuli zake kwa uhakika. Kamati imebaini Mfuko wa Maafa hauna fedha za

kutosha na hivyo kuwepo kwa changamoto kadhaa ambazo kimsingi haziwezi kutatuliwa bila ya kuwepo kwa fedha na vifaa vya kutosha.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inachukua fursa hii kuzipongeza Serikali zote mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa juhudi zao za kuhakikisha wananchi wote wameishi katika maisha ya staha na wamepata nafuu kutokana na ugumu wa maisha. Aidha, shukurani za pekee ziwafikie viongozi na watendaji wote wa Mradi wa TASAF kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kwa namna wanavyoisadia jamii kujikwamua na changamoto za maisha.

**Mheshimiwa Spika,** tunaipongeza Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kutekeleza vyema shughuli zake na kuhakikisha kuwa haki na fursa zote za wajumbe na wafanyakazi zimepatikana kwa mujibu wa taratibu za sheria. Hivyo, Kamati inashauri Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuzidisha kasi ya kusimamia na kufuatilia haki na fursa za watendaji wa Baraza katika kuboresha maslahi yao na kuongeza nguvu ya kuwapatia mafunzo ili kufanya kazi kwa weledi na ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, kamati inashauri Serikali kuharakisha mpango wa kupatiwa gari kwa ajili ya shughuli za Kamati za Baraza kwani mpango huu ulipangwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo hadi kamati inawasilisha ripoti hii hakukuwa na dalili yoyote kuhusiana na upatikanaji wa gari hizo. Maelezo zaidi kuhusu afisi ya Baraza la Wawakilishi yanapatikana Ukurasa wa 44 na 45.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, kamati inashauri Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuharakisha mradi wa ujenzi wa Afisi za Wilaya kwani baadhi ya Wilaya tayari zimepata viwanja kwa ajili ya ujenzi. Aidha, Serikali ni vyema kuongeza nguvu

ya Tume kwa kuwapatia watendaji wa kutosha, kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi. Hata hivyo, kamati inaipongeza Serikali kwa kuwapunguzia Tume changamoto ya usafiri kutokana na kupatiwa gari mpya na za kisasa ambazo zitawasaidia kutimiza malengo ya ofisi.

## 2.4 OFISI YA RAIS – KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

**Mheshimiwa Spika,** ufafanuzi kuhusu Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora unapatikana katika Ukurasa wa 47 hadi 81 ambapo afisi hii imegawika katika sekta kuu tatu; Sekta ya Sheria, Sekta ya Uratibu wa Utumishi wa Umma na Sekta ya Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imeridhishwa na utekelezaji wa ofisi kwa kusimamia vyema majukumu yake na kutoa miongozo kila inapostahiki juu ya masuala ya sheria na utumishi. Kamati inashauri Serikali kufuatilia zaidi utendaji wa Tume za Utumishi na kuzitaka kufuatilia na kusimamia watumishi wao katika kutoa huduma bora kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, kamati imeridhishwa na utendaji wa Taasisi za Dini katika kujenga amani na mshikamano kwa waumini wa Dini ya Kiislamu pamoja na kuhakikisha amani na utulivu wa nchi yetu umelindwa kwa misingi ya Dini zote. Vile vile, kamati inaipongeza Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake na kuhakikisha migogoro ya Dini imepungua kutokana na hatua mbali mbali zinazochukuliwa katika kukabiliana na changamoto za waumini. Hata hivyo, Kamati inaigiza Ofisi ya Mufti Mkuu Zanziba kuendelea kuchukua hatua na kutoa miongozo ya kidini wakati wote wanapoona inafaa kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kujenga misingi bora ya haki na mustakbali bora wa nchi yetu, kamati inaishauri Serikali kuzitumia Taasisi za kusimamia Haki jinai kwa kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai na

uwezo wake wa kuendesha kesi za udhalilishaji katika jamii na athari za kuacha kutumia sheria katika masuala ya kijamii. Kamati inatoa wito kwa jamii kuendelea kuvitumia vyombo vya sheria kuwasilisha changamoto zao hususan kesi za udhalilishaji na kuacha mazoea ya kumaliza kesi hizo katika ngazi za familia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Utumishi wa Umma, kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya upotevu wa majalada ya watumishi au baadhi ya taarifa muhimu kwa baadhi ya wastaafu waliotumikia utumishi wao zaidi ya taasisi moja katika Serikali na kukosekana kwa baadhi ya vielelezo muhimu katika majalada ya wastaafu mfano; mikataba, ardhilhali, barua za vizuizi vya mishahara, vithibitisho vya kifo, barua za bodi ya madaktari na kadhalika. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kupitia Tume za Utumishi kuhakikisha suala hili limesimamiwa ipasavyo na kutafuta suluhisho la upotevu wa taarifa za watumishi Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa sote tunaelewa kwamba jukumu la msingi la Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni kusimamia Maadili ya Viongozi kama Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma inavyoelekeza. Jukumu la kusimamia Maadili ya Viongozi sio la Tume pekee bali ni la wananchi na viongozi wote kwa ujumla. Kwa msingi huo, kamati inashauri kuwa mafaniko ya utekelezaji wa majukumu ya Tume yanahitaji kupata ushirikiano kutoka kwa wananchi, viongozi, sekta binafsi, jumuiya za kiraia na kidini pamoja na vyombo vya habari.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imeelezwa kuwa ujenzi wa Chuo cha Utawala wa Umma Tawi la Pemba unatarajiwa kuanza mwaka huu wa fedha 2023/2024 ambapo chuo kilipanga bajeti ya milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi huo kwa mujibu wa mahitaji ya awali. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya mahitaji halisi ya bajeti iliyotengwa haikuweza kutosheleza. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu ya kusimamia chuo hicho kwa kufanya mazungumzo na taasisi za fedha ili kuona jinsi gani zitaweza kuwajengea na kufanya malipo baadae kwa mujibu wa makubaliano ya kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika Utekelezaji wa Kazi zake ilipata fursa ya kufanya

ziara fupi  za kujifunza jijini Dodoma na Dar es Salaam katika taasisi mbali mbali ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Taifa Mashtaka, Chuo cha Utumishi Magogoni, taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na Sekriterieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

## 2.5 OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

**Mheshimiwa Spika,** maelezo kuhusu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ yanapatikana Ukurasa wa 82 hadi 122 ambapo kamati imeridhika na utendaji wa taasisi zote zilizo chini ya ofisi hii kwa namna zinavyotekeleza majukumu yake. Shukurani za pekee ziende kwa Idara Maalum za SMZ kwa juhudi zao za kulinda na kuendeleza amani na utulivu nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imeridhishwa na mpango wa Serikali wa kuwajengea ofisi za kudumu masheha wote wa Zanzibar, jambo ambalo litaongeza ari ya uwajibikaji kwa masheha wetu. Aidha, kamati inaishauri Serikali kusimamia zoezi la ujenzi wa ofisi hizi kwenda kwa haraka na kuweza kukamilika kabla ya uchaguzi wa mwaka 2025 kwa kuzingatia zaidi kuwa shehia nyingi zimeshapata viwanja na mkandarasi wa ujenzi ameshapatikana.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imebaini kuwa Halmashauri nyingi na Mabaraza mapato yake yameshuka kwa mwaka wa fedha 2023/2024 huku ikielezwa kuwa kuondolewa kwa vyanzo vya mapato ya mali zisizorejesheka katika Serikali za Mitaa ni miongoni mwa sababu za kushuka kwa mapato hayo. Kamati inaishauri Serikali kuziagiza mamlaka zinazohusika na kutoa mgawanyo wa fedha za maliasili na kuzipatia Mamlaka za Serikali za Mitaa fedha hizo kwa wakati ili kuingizwa katika mipango ya bajeti husika.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, kamati imebaini kuwa changamoto ya usafi

haijapatiwa ufumbuzi katika Manispaa zetu za Unguja na Pemba. Hivyo, tunaishauri Serikali za Mitaa kuzidisha kasi ya usimamizi wa usafi kwa kuhakikisha wanatekeleza vyema jukumu la usafi katika maeneo yao. Pia, kamati inazitaka Halmashauri na Mabaraza kutoa fursa kwa kampuni za ndani na nje kuwekeza katika ukusanyaji wa taka kwa lengo kuongeza kasi ya usafi wa miji yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara Maalumu za SMZ, kamati inashauri Serikali kuupitia upya mkataba wa ushirikiano baina ya Serikali ya Misri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuangalia maslahi ya nchi kupitia JKU kwani mkataba huu umeisha muda wake na haujawahi kufanyiwa mapitio. Sambamba na hilo, kamati inapata mashaka kuwa mkataba huu haukuzingatia maslahi ya JKU kwa upande wa Zanzibar na badala yake unazidi kuikandamiza JKU kwa kutumia rasilimali zake bila ya kuwepo kwa faida yoyote.

**Mheshimiwa Spika,** kamati pia, haikuridhishwa na biashara ya uzalishaji na uuzaji wa miwa kwa kikosi JKU na Chuo cha Mafunzo Zanzibar katika kambi mbali mbali za Unguja. Hivyo, tunaiomba Serikali kuangalia upya makubaliano kati ya mnunuzi na muuzaji wa bidhaa hii kwa manufaa ya pande zote mbili.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhishwa na hali ya uchakavu wa gereza la Wete sambamba na miundombinu iliyopitwa na wakati katika magereza mbali mbali. Vile vile, kamati inasikitishwa na hali ya kuwepo mrundikano mkubwa wa mahabusu katika gereza la Kiinua Miguu pamoja na ugumu unaopatikana katika shughuli za Chuo kutokana na kuongeza kwa gharama za uendeshaji. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kufanya utaratibu wa kulihamisha gereza la Kiinua Miguu na kulipeleka Hanyegwamchana kutokana na uchakavu mkubwa na ukongwe wa gereza hili. Aidha, Kamati inashauri kutumiwa Chuo cha Hanyegwamchana kama gereza kuu la Zanzibar kwa kupatiwa miundombinu yenye kukidhi vigezo vya kisasa vya gereza.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hayo, Serikali iweke mkazo katika kuwapatia Chuo cha Mafunzo fedha za matumizi ili kuweza kutoa huduma kwa mahabusu na wanafunzi waliopo magerezani sambamba na kusaidia kuongeza kasi ya kuibua miradi mipya ambayo itapunguza changamoto ya fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuchukuliwa hatua za mara kwa mara katika

kuyatembelea magereza ya watoto na kujua maendeleo yao pamoja kuhakikisha kesi za watoto zinapungua kwa kujenga mashirikiano mema kati ya Wazazi, Mahakama na Chuo cha Mafunzo. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuielimisha jamii juu ya malezi bora ya watoto kwa kupunguza mashauri yanayofunguliwa dhidi ya watoto pamoja na kuifanya jamii kuwa na watoto bora wenye kufuata mila na desturi za kizanzibari.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji wa Idara Maalumu kwenye sekta ya ulinzi wa doria za baharini na nchi kavu, changamoto ya mafuta katika vyombo vya usafiri ni lazima ipatiwe suluhisho la muda mrefu. Kwa mantiki hiyo, kamati inaishauri Serikali kuweka fungu maalumu la mafuta kwa vyombo vya KMKM, KZU na KVZ katika kuendeleza doria kwani kufanya hivyo kutasaidia kufikia msingi wa kazi zao katika kupambana na matukio ya kihalifu.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaishauri Serikali kusimamia ukamilishaji wa mradi ya ujenzi wa nyumba za maafisa na mahanga ya askari wa KMKM katika kisiwa cha Fundo na Kisiwa Panza Pemba kutokana na kutelekezwa kwa mradi huu kwa muda mrefu, licha ya hatua kubwa ya ujenzi iliyofikiwa na kuanza kutumika kwa baadhi ya majengo.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inashauri Serikali kuchukua hatua stahiki kwa Kampuni ya Zenji Holding Co. Ltd ambayo imeshindwa kwenda sambamba na matakwa ya mkataba wa usambazaji wa vifaa kwa Kikosi cha Valantia Zanzibar na kupelekea Mradi wa Ujenzi wa  Nyumba za Maafisa na Mahanga ya Askari Kikungwi kushindwa kukamilika kwa wakati na kusababishia kikosi hasara. Aidha, kamati inashauri mkandarasi huyu kurejesha fedha za Serikali ambazo alipatiwa na hakuzifanyia kazi bila kuonewa muhali kwani kufanya hivyo kuzitafanya Idara Maalumu kuweza kuheshimiwa wanapofanya mkataba wa makubaliano na kampuni binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kujisajili katika matukio ya kijamii na

kuchukua vitambulisho au vyeti kwa wakati kwa wale wananchi wanaojisajili ili kuondokana na mrundikano mkubwa wa vyeti na vitambulisho katika ofisi za wakala.

Kadhalika, kamati inazitaka Taasisi zisizo za Kiserikali kuongeza juhudi katika kutekeleza majukumu yao na kuhakikisha hawaendi nje ya malengo ya jumuiya husika. Aidha, serikali isichoke kuchukua hatua kwa jumuiya yoyote yenye kwenda kinyume na malengo ya katiba zao.

## 3. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla kamati yetu inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Taasisi zote ambazo zipo chini ya Kamati hii kutokana na mashirikiano yao makubwa tunayoyapata kutoka kwa viongozi wa Taasisi hizo, akiwemo Mhe. Ali Suleiman Ameir; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu. Mhe. Harusi Said Suleiman; Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Hamza Hassan Juma; Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Mhe. Mwalim Haroun Ali Suleiman; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, pamoja na Mhe. Masoud Ali Mohammed; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika,** kamati pia inaomba kuwashukuru Makatibu wakuu na Wakurugenzi wote wa Taasisi hizi, Makamanda wa Idara Maalum, wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wote wa Zanzibar na Makamishna kwa ushirikiano wao mkubwa walioipatia kamati wakati wa kazi zake. Kamati inawashukuru watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakiongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndugu Raya Issa Mselem, pamoja na Mkuu wa Idara ya Baraza la Wawakilishi Pemba Ndugu Abdul-ghani Abdullah Said kwa ujasiri wao wa usimamizi na kuleta mabadiliko katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inashauri viongozi wa Wizara na taasisi zote zinazosimamiwa na Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa

kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika ziara za kamati, kutokufanya hivyo kutapelekea kushindwa kupokea taarifa zao kwa usahihi na zenye kuaminika. Aidha, kamati inaziomba Wizara na Idara zote zinazohusika kuyachukua maoni, ushauri na mapendekezo ya ripoti na yale yatayotokana na michango ya wajumbe kwa kuyafanyia kazi na kuja kuyatolea ufafanuzi wa kuridhisha ikifika kikao cha Mwezi wa Septemba kama Kanuni ya 109 (17) ya Baraza la Wawakilishi, toleo la 2020 inavyoelekeza.

Kwa kumalizia, napenda kukushukuru tena Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii na pia, nawaomba Waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili Tukufu kuisoma na kuichangia ripoti hii kwa umakini.

**Mheshimiwa Spika,** **Naomba Kutoa Hoja.**

**Ahsante;**

……………………………………

**(Machano Othman Said)**
**Mwenyekiti;**
**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa**
BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR